



# OR-TAMISEMI



*Uboreshaji wa huduma za afya hapa Nchini  
Maboresho yanayoendelea*

**Kikao cha Waganga wakuu wa Mikoa na  
Wilaya-Ukumbi wa LAPF  
DODOMA 13-18/08/2018**



# MTIRIRIKO WA MADA

- **Tumetoka Wapi?**
- **Tuko wapi?**
- **Tunataka kwenda wapi?**
- **Mikakati ya kufikia Malengo**



# UTANGULIZI.....

- **Ili kuelekea uchumi wa kati na Maendeleo ya viwanda**
  - Nchi inahitaji nguvukazi (wananchi) imara
  - Nguvu kazi imara inahitaji afya bora
  - Afya bora inapatikana kwenye mazingira bora ya kutolea huduma za afya
  - Uboreshaji wa Mazingira Bora ya kutolea huduma za afya
  - ✓ Msingi wa wananchi kufikia uchumi wa kati na maendeleo ya viwanda



# I. TUMETOKA WAPI?

- Ziara ya pamoja kati ya OR-TAMISEMI, WAMJW na WFM Mwezi Nov 2016
- Ziara ilibaini Mazingira duni ya kutolea huduma za afya
  - Uchakavu wa majengo ya kutolea huduma za afya
  - Uchache wa Miundombinu ya huduma za afya
- ✓ Halmashauri 184, Hospitali (W) (108 za Serikali 77)
- ✓ Kata 4,420 vituo vya afya 518 (12%)
- ✓ Vijiiji 12,545 Zahanati 4,554 (36%)
- Maboma 1,845 yanayohitaji zaidi ya shilingi mil. 900 kuyakamilisha



# Tumetoka Wapi?.....

- **Upungufu wa watumishi**
  - Mahitaji 119,562 Waliopo 55,881 Upungufu 63,681
  - Zahanati 180 zimekamilika lakini hazijaanza kazi
  - Zahanati 380, zinaendeshwa na wahudumu wa afya
  - Zahanati 1,400 hazina waganga zinaongozwa na wauguzi au Maafisa wauguzi wasaidizi



# Hii ndio emergency room kwenye vituo vyetu





# Hii ndiyo hali ya vitanda vyetu vya kujifungulia





# Vyoo vya watumishi na wagonjwa ndio hivi





# NINI KIMEFANYIKA (TUKO WAPI?)

- Baada ya ziara Taarifa iliandaliwa
- Kulikuwa na Maazimio yaliyotokana na ziara
- Taarifa ilisambazwa Wizara zote zinazogusa sekta ya afya
  - ✓ WAMJW
  - ✓ OR-TAMISEMI
  - ✓ WFM
  - ✓ OR-UUB
- Mpango Mkakati wa pamoja wa Uboreshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya Uliandaliwa na kuhusisha Wizara zote.



# Vipaumbele vya Mpango Mkakati wa Uboreshaji wa Huduma za Afya

- I. Ukarabati wa vituo vya afya vyote ili viweze kutoa huduma za Dharura kwa akina mama Wajawazito
2. Ukarabati wa Zahanati 2,277 (angalau nusu ya zilizopo)
3. Kukamilisha Maboma 1,845 ifikapo 2020 ili yaanze kutoa huduma
4. Kujenga Kimkakati vituo vya afya na Zahanati:
  - Angalau vituo vya afya 599 kwenye halmashauri zisizo na vituo
  - Zahanati 1,719 ili kufikia angalau 50% ya kila kijiji kuwa na zahanati



## **Vipaumbele vya Mpango Mkakati wa Uboreshaji wa Huduma za Afya**

5. Kujenga Hospitali za Wilaya 67 kwenye Halmashauri ambazo hazina Hospitali za Wilaya
6. Kuomba OR-UUB watumishi 35,000 wa kutolea huduma za afya
7. Kuboresha huduma za afya (mipango ya afya ya vituo) kwa kupitia Mkakati wa DHFF
8. Kuboresha taarifa za Afya kwa kupitia Mifumo ya TEHAMA (FFARS, DHIS2, GoT-Homis)



# **Utekelezaji wa Mpango Mkakati/Mafaniko yaliyopatikana**

Mabadiliko yafuatayo yametokea 2017/2018 kufuatia  
Uwajibikaji wa pamoja Wizara zote na wadau

## **I. Ukarabati wa vituo 307 unaendelea**

- Awamu ya Kwanza vituo 44 Okt, 2017-Jan, 2018
- Awamu ya pili vituo 139 Jan-Mei, 2018
- Awamu ya tatu vituo 27 Mei-Okt, 2018
- Awamu ya 5 vituo 97-LGCDG-Jun-Des

**2. Bajeti ya 2018/2019 TZS 100.5 Bilioni zimetengwa  
kujenga Hospitali 67 za Wilaya-Kupitia fedha za LGCDG**



# **Utekelezaji wa Mpango Mkakati....**

## **3. Kuongezeka kwa Rasilimali watu vituoni**

- Watumishi 8,494 wameajiriwa na kupelekwa vituoni

## **4. Uimarishaji wa usimamizi wa Matumizi ya fedha**

- Utaratibu wa upelekaji wa fedha Moja kwa Moja vituoni (DHFF umeanza)
- Utumiaji wa mfumo wa FFARS kudhibiti fedha za vituo umeanza



# **Uwajibikaji wa Pamoja umeleta Matokeo Chanya**





# Ukarabati wa vituo-Kwa Pamoja Mafanikio yamepatikana





# Mambo Mazuri ya Kujifunza

1. Matumizi ya “force account” yamepunguza gharama za ujenzi (kamati tatu)
2. Ushirikishwaji wa wananchi umemilikisha mchakato wa ujenzi kwa wananchi
3. Uongozi na usimamizi imara kutoka ngazi zote ni chachu ya mafanikio
4. Ushirikiano wa pamoja kati ya Serikali, Wananchi na Wadau wa maendeleo ni nguzo ya mafanikio



# Ushirikishwaji wa Jamii kumiliki Mchakato wa Ujenzi





# **Wadau wetu wa Maendeleo tunatembea nao pamoja kwenye utekelezaji**





# Muelekeo ni upi (Tunakwenda wapi)?

- **Agenda yetu kuu:**
- Kuunga Mkono juhudi za Mhe. Rais wa JMT Dkt. John Pombe Magufuli kwa utekelezaji wa Ilani ya chama cha Mapinduzi ibara ya 50 (a) i, vii-ix; h, (j), (q)i-v.
- ✓ Kwa kufanya uboreshaji na uongezaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya
- ✓ Kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba
- ✓ Kuongeza upatikanaji wa watumishi vituoni na kuwapa motisha
- ✓ Kuweka utaratibu wa Bima ili wananchi wamudu gharama za Matibabu





# Muelekeo ni upi (Tunakwenda Wapi?)....

## Agenda yetu kuu:

- **Kuboresha na kuongeza miundombinu ya kutolea huduma za afya hapa Nchini**
  - Kukamilisha ukarabati wa vituo vya afya 289
  - Kukarabati zahanati 2,277 (nusu ya zilizopo)
  - Kujenga kimkakati zahanati 1,719 na vituo vya afya 592
  - Kujenga Hospitali za Wilaya 67
  - Kukamilisha maboma 1,772 (1,845)
- Kuongeza watumishi wenye sifa vituoni
- Upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba uwe asilimia 100



# MIKAKATI YA KUFIKIA MALENGO

- Kuimarisha mahusiano na uratibu wa wadau ngazi zote
- Mipango yote kuingia kwenye CCHP na fedha kupelekwa vituoni kupitia mkakati wa DHFF
- Kuendelea kuajiri watumishi wenyе sifa kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya (2018/19-25,822)
- Kuimarisha makusanyo ya fedha zitokanazo na huduma
- ✓ Kuimarisha makusanyo ya fedha kupitia iCHF
- ✓ kukamilisha taratibu za kuelekea kwenye Mfumo wa Bima moja ya Taifa (single National Health Insurance)
- Kuimarisha huduma za afyakinga na mahusiano kati ya Jamii na vituo vya kutolea huduma za afya.



# Tukishirikiana kwa Pamoja, Tutaleta Mabadiliko na kufikia uchumi wa kati na Maendeleo ya Viwanda





**Ahsanteni kwa Kunisikiliza**